



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



Septemba 14, 2022

### TAARIFA KWA UMMA

#### MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA AMEONGOZA KIKAO CHA WADAU WA KILIMO WILAYANI LUDEWA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias akiwakilishwa na Castor Kibassa ambaye pia ni Afisa Mazingira Wilaya ya Ludewa ameongoza kikao kazi cha wadau wa Kilimo ambaao ni Shirika lisilo la kiserikali linalojukana kwa jina la **CARE INTERNATIONAL** na Kampuni ya **MY AGRO**.

Kikao hicho kimefanyika katika ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya ya Ludewa, pamoja na mambo mengine wamejadili mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kuwafikia wakulima wa Kata 7 na vijiji 16 kama ifuatavyo, Kata ya Mavanga, Mundindi, Mkomang'ombe, Luilo, Masasi, Manda na Ruhuhu.

Kata hizo ndizo zitakazo nufaika na mradi huo wenyе jina la **CARE MY AGRO** wenyе lengo la kuwapa elimu wakulima na kuwapa pembejeo haswa katika mazao ya Alizeti, Karanga na Mbogamboga.

Bi. Monica Gachara akitokea nchini Kenya ambaye pia ndiye Msimamizi wa Mradi huo akiambatana na Bi. Hawa Omary akitokea Dar es salaam ambaye pia ni Afisa wa Mradi huo wameahidi kushirikiana na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwawezesha wakulima kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini na ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa haswa katika mazao ya mkakati wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhamasisha na kuwafundisha wananchi kulima mbogamboga kwa lengo la kuimalisha lishe ndani ya kaya na kutokomeza Uduvalu.

Chrispin B. Kalinga  
Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini  
Halmashauri (W) Ludewa.